KIGOMA HABARI ZA MKOA

News Bulletin

Web: http://www.kigoma.go.tz

Toleo Na. 005 Habari za Kila Mwezi 31 Julai

# Watanzania Jitokezeni Kushiriki kujiandikisha kwenye Daftari la kudumu la Wapiga Kura



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzana Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akibonyeza kifaa Maalumu kuashiria kuanza rasmi kwa Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Mpiga Kura Mkoani Kigoma*

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amezindua zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura huku akiwataka watanzania wote kujitokeza kujiandikisha na kuboresha taarifa zao katika daftari hilo.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo wa daftati la kudumu la wapiga kura uliofanyika uwanja wa Kawawa manispaa ya Kigoma Ujiji Waziri Mkuu Majaliwa alisema kuwa zoezi la uboreshaji wa daftari kudumu la Wapiga kura na zoezi zima la Wapiga kura linawuhusu watanzania kulingana na kutambuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema kuwa taarifa za tume huru ya Taifa ya uchaguzi (INEC) inaonyesha kuwepo kwa wapiga kura wapya milioni 5.5 ambao wanapaswa kuandikishwa kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 hivyo tume imejiandaa kuhakikisha watu wote hao wanaandikishwa katika zoezi la kuandikisha.

Sambamba na hili Waziri Mkuu Majaliwa amewataka Viongozi na Watendaji wote kusimamia kwa karibu utekelezaji wa zoezi hilo wakiwemo mawakala kuhakikisha wanaondikishwa kwenye daftari la kudumu la wapiga kura ni Watanzania ili wapate nafasi ya kuchagua viongozi wao na kuwafichua watu ambao siyo watanzania wanaotaka kujipenyeza kuandikishwa.

# Majaliwa awasisitiza Wananchi kujitokeza Daftari la Mpiga Kura

Aidha Waziri Mkuu Majaliwa pia ameyaasa mashirika yasiyo ya serikali yaliyoteuliwa kutoa elimu kwenye zoezi la uandikishaji na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kuzingatia majukumu yao kulingana na maombi yao na zoezi lenyewe badaya la kufanya mambo ambaayo hayasiaani na taratibu za daftari wala uchaguzi.

Katika uzinduzi wa zoezi hilo Waziri Mkuu Majaliwa alitoa agizo kwa idara ya uhamiaji mkoa Kigoma na nchi nzima kwa jumla kutembelea vituo na kufanya uhakiki wa watu wanaoandikishwa kuwa ni Watanzania na kufanya kazi taarifa watakazopata kuhusu watu wanaotaka kujiandikisha ambao siyo Watanzania.

Mwenyekiti wa Tume huru ya Taifa ya uchaguzi nchini (INEC), Jacob Mwambegele alisema kuwa Katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka huu 2024 kutakuwa na jumla ya vituo 40,126, ambapo kati ya vituo hivyo, 39,709 ni vya Tanzania Bara na vituo 417 ni vya Zanzibar.

Awali akitoa taarifa kwa Waziri Mkuu, Mwenyekiti wa Tume huru ya Jaji Mwambegele alisema kuwa hilo ni ongezeko la vituo 2,312 ikilinganishwa na vituo 37,814 vilivyotumika kuandikisha wapiga kura mwaka 2019/2020 huku kukiwa na ongezeko la wapiga kura wapya milioni 5.5,wapiga kura milioni 4.3 wataboresha taarifa zao na wapiga kura



*Mwananchi akipatiwa huduma ya Kitambulisho cha mpiga kura baada ya zoezi kuzinduliwa na Waziri Mkuu katika Viwanja vya Kawawa manispaa ya Kigoma Ujiji Mkoai Kigoma*

594,494 wataondolewa kwenye Daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwepo kwenye Daftari hivyo baada ya uboreshaji inatarajiwa kuwa Daftari litakuwa na jumla ya wapiga milioni 34.7.

Aidha katika uzinduzi huo Waziri Mkuu Mkuu amevitaka vyama vya siasa ambao ndiyo wadau wakubwa wa uchaguzi huo kutoa elimu kwa wanachama wao kuhusu zoezi hilo lakini pia kuweka mawakala ambao watasimamia zoezi hilo kwenye vituo akitaka mawakala hao kutolewa kwenye maeneo husika ya vituo na kuwa na uzalendo na nchi yao.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 005 Habari za Kila Mwezi 31 Julai 2024

# TAHARIRI

Katika kipindi cha Takribani miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Afya imetazamwa kwa jicho la tofauti na kufanikiwa kupiga hatua kubwa kimaendeleo kwa lengo la kuharakisha, kurahisha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za Afya mkoani Kigoma na Taifa kwa ujumla.

Maendeleo hayo yamegusa katika uboreshwaji mkubwa wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya, kuongeza Ikama ya watoa huduma pamoja na ongezeko kubwa la upatikanaji wa vitendanishi na vifaa tiba, ubora wa huduma na usimamizi madhubuti wa Sekta hiyo.

Lengo la serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha Huduma za Afya mkoani Kigoma ni kuhakikisha Wananchi wanapata matibabu sahihi na kwa wakati, kutoa elimu ya kujikinga na maradhi, kubaini maradhi katika hatua za awali, kutoa kinga tiba pamoja na kuboresha maisha kwa kuisaidia jamii kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kuishi mazingira salama kiafya.

Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2024, mkoa wa Kigoma umepokea jumla ya Shilingi 19,054,052,429 kutoka serikalini kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya ambapo jumla ya Shilingi 16,794,417,133.83 zimetumika katika kutekeleza miradi ya ujenzi na Shilingi 2,259,635,295.00 zimetumika kwa ajili ya manunuzi ya vitendanishi na vifaa tiba.

Miradi ya ujenzi iliyotekelezwa mkoani Kigoma ni pamoja na ukarabati wa Hospitali Nane za Halmashauri, ujenzi na upanuzi wa vituo 16 vya Afya, umaliziaji wa maboma katika Hospitali, vituo vya Afya na Zahanati katika halmashauri hizo pamoja na ujenzi wa nyumba 26 za watumishi katika halmashauri zote nane za mkoa..

Aidha kazi nyingine zilizotekelezwa ni ujenzi wa kituo cha Damu Salama katika Hospitali ya Mkoa wa Kigoma Maweni, uimarisha wa huduma za msingi za matokeo, ujenzi wa majengo ya huduma za dharura katika hospitali za wilaya Kibondo, Uvinza, Kakonko na Buhigwe.

Ongezeko la upatikanaji wa vifaa tiba pamoja na vituo vya kutolea huduma za Afya linachangia kupunguza idadi ya wakazi wanaotegemea mitishamba kimatibabu au kuamini katika ramli chonganishi hali iliyokuwa ikisababishwa na uhaba wa vifaa vya kufanyia vipimo sahihi vya magonjwa mbalimbali wanayougua kwa muda mrefu..

kuongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 288 kwa mwaka 2022 hadi kufikia 332 kwa mwaka 2024 hali hii imewezesha kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 102 hadi kufikia 29 huku vifo vya watoto wachanga vikipungua kutoka 727 hadi 287 .

mafanikio mengine ni kuimarika kwa hali ya utoaji wa huduma ambapo katika kipindi cha miaka mitatu mkoa umepokea jumla ya watumishi wa kada ya afya 950 sawa na 67% kutoka 60% ya waliokuwepo awali.

Kuhusu mapambano dhidi ya maradhi ya ukimwi, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2022 hadi 2024, kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo kimeshuka kutoka 2.7% hadi kufikia 1.7% sambamba na uwepo wa ufuasi mkubwa miongoni mwa wenye VVU.

Katika kipindi hicho cha miaka mitatu, mkoa umefanikiwa kuanzisha Huduma za M-mama kwa ufanisi mkubwa pamoja na kupokea magari ishirini na mawili kwa ajili ya kubeba wagonjwa na kufanya usimamizi shirikishi wa huduma za afya mkoani Kigoma.

Kuimarika kwa mifumo ya kutolea huduma za Afya mkoani Kigoma kunakoendana na kusheheni kwa vifaa tiba, watoa huduma mahiri pamoja na ujirani wa maeneo ya kutolea huduma za afya ni jambo la kujivunia na kushukuru kupitia utimilifu wa maono ya kion gozi mkuu wa taifa katika kuhakikisha huduma hizo muhimu zinawafikia wananchi kwa usahihi na wakati..

# Watendaji Idara ya Afya Mkoa wa Kigoma Wapewa Neno

Katibu Tawala mkoa wa Kigoma Hassan Abbas Rugwa amewakumbusha watendaji wa Serikali walio chini ya Idara ya Afya mkoani Kigoma kuzingatia maelekezo na maaagizo m balimbali yanayotolewa na serikali ikiwemo agizo la kutoendelea kutoza fedha kwa ajili ya kulipia kadi za Kliniki pamoja na faini kwa wanawake wanaojifungulia nje ya vituo vya kutolea Huduma za Afya.

Hayo yamejiri kufuatia katibu Tawala huyo kukutana na kuzungumza na watendaji wa Idara hiyo kwa lengo la kuwahimiza kuhusu kusimamia utekelezaji wa agizo hilo lililotolewa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango alipofanya ziara yake ya kikazi mkoani Kigoma na kuiagiza Wizara ya OR-TAMISEMI kuchukua hatua madhubuti ili kudhibiti suala hilo.



*Ndg. Hassan Abbas Rugwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma*



*Watumishi wa Idara ya Afya wakifuatilia Maelekezo ya Viongozi Mkoani Kigoma*

Ifahamike kuwa, agizo hilo lilikuja kufuatia baadhi ya wakazi katika Wilaya za Uvinza na Kasulu kutoa malalamiko kwa kiongozi huyo kuhusu kutozwa fedha katik ya Shilingi 30,000 hadi 50,000 kutokana na kujifungua nje ya kituo cha kutolea huduma za Afya sambamba na kulipia kadi za Kliniki.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Dkt. Ibrahim Salehe amesema Idara ya Afya Mkoa wa Kigoma kwa kushirikiana na watendaji wake katika ngazi za Halmashauri imeshaanzan kutekeleza agizo hilo ikiwemo kuchapisha kadi za kutosha na kuzigawa kwa wanawake wanaojifungua kupitia vituo vyote vya kutolea huduma za Afya.

Aidha amesisitiza kuwa Ofisi ya Mganga Mkuu Mkoa haitosita kuchukua hatua dhidi ya watumishi watakaokaidi kutekeleza agizo hilo ili kuruhusu utoaji wa huduma hizo bila kuwepo kwa aina yoyote ya kikwazo.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz

Toleo Na. 005 Habari za Kila Mwezi 31 Julai 2024

# Kigoma yaweka Mikakati Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Jenerali Mstaafu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Thobias Andengenye amewataka watendaji katika Taasisi za Umma na Halmashauri mkoani hapa kuongeza ubunifu katika kubaini vyanzo vya mapato ili kuongeza kuinua kiwango cha makusanyo katika Halmashauri na kuziwezesha kumudu kujiendasha sambamba na kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo.

Mhe. Andengenye ametoa kauli hiyo alipozungumza kwenye Kikao kilichowakutanisha wataalam kutoka Taaasisi za Umma pamoja na watendaji kutoka mamalaka za serikali za mitaa mkoani hapa kikilenga kujadili na kubaini fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo kwenye mkoa wa Kigoma na kupanga mikakati ya namna bora ya kuzitumia ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Amesema mko una vyanzo vingi vya Mapato, kinachotakiwa ni ubunifu katika ubainifu wa vyanzo hivyo ili viweze kuleta tija katika uzalishaji na ukusanyaji wa mapato, jambo litakaloimarisha uchumi wa mkoa na nchi kwa ujumla.

Aidha Mkuu huyo wa Mkoa amewataka watendaji hao kujenga utamaduni wa kutoa huduma bora kwa wananchi jambo litakalowezesha wapokea huduma kuzitangaza kazi nzuri zinazofanywa na serikali mkoani hapa.



*Baadhi ya Washiriki wa Kikao Kazi cha Wakurugenzi na Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa*

Amesema malengo ya mkoa ni kuhakikisha kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 malengo ya makusanyo kimkoa hadi ifikapo 20230 ni kufikia kati ya shilingi Bil.20 hadi 25.



*CGF (Mst.) Thobias Andengenye Mkuu wa Mkoa wa Kigoma*

Aidha Rugwa amewataka watendaji hao kwenda kuibua vyanzo vipya vya mapato katika maeneo yao wanayoyasimia na kuondoa vya"Hakikisheni mnaandaa mazingira bora ya ukusanyaji wa mapato, kuondoa tozo zinazoweza kuwaletea kero wananchi sambamba na kuandaa mazingira yatakayotoa fursa kwa wawekezaji ili waweze kuwekeza katika maeneo yenye vivutio vya uwekezaji" amesema Rugwa.

Upande wake Mkuu wa Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mkoa Ndg. Deogratius Sangu amesema kikao hicho cha wataalam wa mkoa kimehusisha wakuu wa Taasisi za Umma zilizopo mkoani humo, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, wachumi, wataalam wa mipango na mipango miji pamoja na Maafisa biashara lengo kuu likiwa kuhakikisha wataalam hao wanajengewa uwezo katika kubaini na kuhakikisha wanatumia vursa za kiuchumi zilizopo mkoani humo kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 005 Habari za Kila Mwezi 31 Julai 2024

# Dkt. Mpango ampongeza RC Andengenye Kuimarisha Uhusiano baina ya Watendaji wa Serikali na CCM




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango akiwa na Viongozi wa Mkoa wa Chama Cha Mapinduzi alipofanya ziara ya kiakazi Mkoani humo*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango amesema mahusiano mazuri yaliyopo baina ya Uongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na uongozi wa Serikali ya Mkoa yamekuwa chachu ya kufikia malengo ya serikali kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo mkoani Kigoma.

Mhe. Dkt. Mpango ametoa kauli hiyo alipokutana na viongozi wa CCM na kusisitiza kuwa, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma amekuwa kiunganishi kizuri baina ya pande mbili hizo kutokana na kufanya kazi kwa uwazi na ushirikishaji.

Amesema kumekuwa na ushirikiano mkubwa baina ya wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa pamoja na viongozi wa ngazi mbalimbali ndani ya CCM, jambo linalowapa fursa wananchi kupata taarifa sahihi kuhusu kazi zinazofanywa na kuendelea kuiamini serikali kupitia ushirikishwaji huo.

"Nitoe pongezi zangu za dhati kwako Mkuu wa Mkoa kutokana na kushirikiana bega kwa bega na viongozi hao ambao ndio wawakilishi wa wananchi katika maeneo yao, jambo linalosababisha kuondoa migogoro na mivutano isiyo ya lazima katika usimamizi na utekelezaji wa kazi mbalimbali za miradi ya maendeleo mkoani hapa" amesema Makamu wa Rais.

Aidha Makamu wa Rais amewataka viongozi hao wa Chama Cha Mapinduzi kuwa wajumbe na mabalozi wazuri katika kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura sambamba na kujitokeza kwenye mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa kwa ajili ya kupiga au kupigiwa kura ili nchi iweze kupata viongozi bora.

Katika hatua nyingine Makamu wa Rais amepongeza uamuzi wa mkuu huyo wa mkoa kwa kwa kuruhusu wananchi wanaodaiwa kulima katika eneo la hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini mwanzoni mwa Mwaka huu, kuwataka kuondoa mazao yao bila kuzuiliwa na watendaji kutoka wakala wa Huduma za Misitu nchini(TFS).

"Haiwezekani mtu analima mnamuacha, anapalilia mnamuangalia tu, wakati wa kuvuna ndipo mnaanza kupambana nae na kumnyang'anya mazao yake kwa kosa la kulima katika eneo la hifadhi, huo ni unyanyasaji mkubwa kwa nini msiwadhibiti wakulima hawa katika hatua za awali ili wasilime kabisa bali mnakuja kuwasumbua wakati wa kuvuna? Hili linafikirisha sana" amesema Dkt. Mpango.

Pamoja na hayo, Makamu wa Rais amempongeza Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu kwa kuendelea kuelekeza fedha nyingi mkoani Kigoma kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya kuboresha maisha ya wakazi mkoani Kigoma.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 005 Habari za Kila Mwezi 31 Julai 2024

# Marufuku Kuwatoza Wajawazito Kadi za Kliniki –Dkt. Mpango

Makamu wa Rais wa Jymhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango amemuagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia kwa Naibu wa Waziri wa Wizara hiyo Zainab Katimba kupitia upya Sheria Ndogo za Sekta ya Afya katrika Halmashauri zinazoruhusu kulipia kadi ya kliniki pamoja na kutoza faini kwa wanaojifungua nje ya vituo vya Afya ili kuzisitisha sheria hizo mara moja.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango akizungumza na Wananchi wa Nguruka-(pichani hawapo)*

Makamu wa Rais ametoa agizo hilo Julai 12, 2024 akiwa

katika ziara yake ya kikazi wilayani Kasulu ambapo amepokea malalamiko ya wanawake kutozwa faini kati ya Shilingi 40,000 hadi Shilingi 50,000 na kusisitiza kuwa kitendo hicho ni kinyume na sheria na utaratibu huo unapaswa kusitishwa.

"Changamoto hii inaonekana kuwepo maeneo mengi ndani na nje ya mkoa wa Kigoma hivyo ninaiagiza Wizara kupitia upya sheria hizo na kuandaa mwongozo wa kuziondoa kisha mzishushe kwenye Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji ili kuhakikisha utaratibu huo haujirudii tena"amesisitiza Dkt. Mpango.

Amesema ni jukumu la watendaji wa serikali kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kujifungua katika vituo vya Afya na inapotokea mjamzito kajifungua nje ya kituo cha kutolea huduma za Afya wahudumu wanapaswa kumpokea na kumpatia huduma bila masherti yoyote

Sambaba na hayo, Makamu wa Rais ameuelekeza uongozi wa wilaya kupitia wakuu wa wilaya kuhakikisha wanatumia mbinu mbadala ili kuhakikisha ukosefu wa vitambulisho hivyo hauwanyimi fursa vijana kupata kazi katika mashirika au taasisi binafsi ili waweze kujipatia kipato.

Katika hatua nyingineDkt. Mpango ameuelekeza Uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA)kutekeleza jukumu lao la kutoa Elimu kwa Jamii badala ya kusumbua wamiliki wa vyombo vya Usafiri hususani waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda

Aidha ameitaka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuongeza kasi katika kushughulikia utoaji wa vitambulisho vya NIDA ili kutoa Fursa kwa wananchi kuvitumia kuendana na matakwa ya Serikali

"Jukumu lenu la Msingi ni kutoa elimu na kuhamasisha watumiaji wa barabara wanazingatia taratibu na miongozo na wale watakaobainika kushindwa kuzingatia taratibu hizo ndio wachukuliwe hatua na sio kushinda mnakamata vyombo hivyo kabla ya kutoa elimu kwa Umma" alisisitiza Dkt. Mpango

# Ujenzi wa Njia ya Umeme Nyakanazi-Kidahwe wafikia 80%

Ujenzi wa njia ya kusafirisha Msongo wa Umeme wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kidahwe wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 434.9 umefikia zaidi ya 80% ambapo kukamilika kwa Mradi huo kunatajwa kuwa suluhisho la kudumu kutokana na mkoa kuwa na changamoto ya muda mrefu ya utoshelevu wa upatikanaji huduma ya Umeme.

Mradi huo unahusisha miradi mitatu ambapo kwa upande wa mradi wa ujenzi wa njia ya Umeme Nyakanazi hadi Kidahwe ulioanza kutekeleza Januari 2022 na Mkandarasi M/s TATA Projects Ltd kutoka nchini India, umefikia 84% na unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba 30, 2024

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Thobias Andengenye amesema Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu amedhamiria kuwaondolea wananchi wa mkoa wa Kigoma adha ya ukosefu



*Kazi ya usimikaji nguzo za kusafirishia Umeme wa Grid ya Taifa ikiendelea katika Maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kigoma*

wa umeme kwa kuidhinisha ujenzi wa mfumo huo utakaoingiza umeme wa kutosha na wenye uhakika katika kuendesha shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

Amesema kukamilika kwa mradi huo kutaipunguzia hasara Serikali kwa kuachana na matumizi ya mafuta yanayofikia kiasi cha lita 30,000 kwa siku kwa ajili ya uendeshaji wa jenereta zinazozalisha Umeme unaotumika mkoani Kigoma

"Matumizi ya jenereta yametupeleka kwenye mgao wa umeme kutokana na kutotosheleza kwa nishati hiyo, jambo lililochangia kwa kiasi kikubwa mkoa kukosa wawekezaji upande wa Sekta ya viwanda jambo linaloikosesha nchi kiasi kikubwa cha mapato" amesema.

'Ifahamike kuwa serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kutoka Tabora hadi Kigoma yenye urefu wa Km. 506, ujenzi wa kiwanda cha kutengenezea Meli pamoja viwanda vingine vilivyopo vya kuchakata bidhaa mbalimbali ambavyo vyote hivyo vitahitaji kuendeshwa kwa kutumia umeme wa uhakika" ameendelea kufafanua Andengenye.

Mhandisi wa ujenzi wa miundombinu ya Usafirishaji wa Msongo wa Umeme Nyakanazi hadi Kidahwe Nyango Magesa amesema kazi za usanifu wa mradi huo zimefikia 99% Manunuzi ya vifaa 99% pamoja na Ujenzi kufikia 84.4%

Ameutaja mradi mwingine unaotekelezwa sambamba na mradi huo ni ujenzi wa njia za usambazaji Msongo wa Umeme wa KV 33 na Voti 400 kwa Thamani ya Shilingi Bil. 11.5 ukitekelezwa na Mkandarasi M/s Giza Cable Industries kutoka nchini Misri pamoja na ujenzi wa Kituo cha kupoza Umeme Kigoma na Kasulu unaotekelezwa kwa Gharama ya Takribani Shilingi Bil. 9.2 ambapo hatua iliyofikiwa ni usanifu wa michoro, uchunguzi wa udongo kwa ajili ya kuona iwapo maeneo husika yanafaa kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo

Vijiji vitakavyonufaika kwa wilaya ya Kasulu ni Makere, Nyachenda, Titye, Kitagata, Nyamidaho, Mvugwe, Nyarugusu, Muzye, Bugaga na Kasangezi ambapo kwa Halamshauri ya Mji ni Kanazi, Nyantare, Nyumbigwa na Bugaga

Mhandisi Magesa amesema zoezi la ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyopitiwa na Mradi huo limekamilika kwa Asilimia 91 ambapo kiasi cha Shilingi Bil. 2.32 kimelipwa kwa wananchi ambao maeneo yao yamepitiwa na mradi na kwa wanaoendelea kuthibitisha taarifa zao watapokea malipo kabla ya mwishoni mwa Mwezi Agosti 2024.

Stephano Gwarema Mkazi wa Kijiji cha Rusesa amesema ameridhishwa na kasi ya serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususani suala la kuimarisha huduma za Umeme, Afya, Maji na barabara katika maeneo ya vijijini.

Kazi zinazoendelea kufanywa na serikali tumeridhishwa nazo na nitoe wito kwa wananchi wenzangu tuendelee kutunza miundombinu hii ili iweze kudumu kwa ajili ya matumizi ya sasa na vizazi vihavyo.

"Mfumo huu wa Umeme unaotekelezwa mkoani Kigoma utakapokamilika utasaidia uwepo wa viwanda vitakavyoweza kutupatia ajira wakazi wa Kigoma na kujiimarisha kiuchumi ili tuweze kumudu kuendesha maisha" amesema Gwarema.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz

Toleo Na. 005 | Habari za Kila Mwezi | 31 Julai 2024

# Kigoma kushirikiana na Wadau Kuinua Kiwango cha Elimu

Serikali mkoani Kigoma imeahidi kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa Elimu ikiwemo Mradi wa Shule Bora ili kuboresha na kuimarisha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji ili kuendelea kuinua ubora wa Elimu.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma Hassan Rugwa alipokutana na kuzungumza na wadau wa Elimu wanaotekeleza mradi wa Shule Bora mkoani Kigoma na kusisitiza kuwa lengo la serikali ni kuona ubora wa Taaluma unaendelea kuimarika kutokana na maboresho ya Mazingira ya utoaji na upataji wa Elimu

Amesema Serikali kupitia watendaji wa Sekta hiyo mkoani hapa wataendelea kushirikiana na wadau ili kupunguza changamoto zinazochangia kuzorotesha na kutofikiwa kwa malengo ya serikali katika utekelezaji wa mipango ya kitaaluma sambamba na mdondoko wa wanafunzi.

Kiongozi wa Programu ya Shule Bora Taifa, Virginie Briand ameeleza kuwa mradi wa shule bora una lengo la kumuwezesha mwalimu kutekeleza majukumu yake kwa usahihi kupitia mafunzo wanayopatiwa sambamba na kusaidia zoezi la upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi wakiwa shuleni ili kufanikisha zoezi la ujifunzaji na ufundishaji

Amesema kwamba vyumb vinavyotumika kutolea Elimu lazima viakisi picha halisi ya Mazingira ya ujifunzaji hali itakayopelekea kupunguza utoro na kuwafanya wanafunzi kuhudhuria vipindi madarasani bila kutoroka na kuhakikisha walimu na wazazi wanasimamia zoezi la upatikanaji wa chakula kwa watoto ili kuhakikisha watoto wanapata utulivu muda wa kujifunza.

Akizungumza na watendaji na wadau wa Sekta ya Elimu katika Kata ya Kidahwe, wilaya ya Kigoma, Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu Msingi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Susana Nussu amewataka wazazi kushirikiana na walimu kwa kufuatilia mahudhurio ya watoto na kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali kupitia miradi ya Elimu ya Kujitegemea (EK) iliyopo katika mazingira ya shule.

Bi. Susana amewakumbusha walimu mkoani Kigoma kujenga utamaduni wa kufanya Tathmini za mara kwa mara wakati wa ufundishaji na baada ya ufanyikaji wa mitihani ili kutambua maeneo yenye changamoto na mafanikio kisha kuchukua hatua ikiwemo kurudia mada, kutoa mazoezi ya kutosha kwa lengo la kuimarisha uelewa wa wanafunzi wao.



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma Ndg. Hassan Abbas Rugwa*

Aidha, Sasana amesema kuwa mbinu jumuishi za ufundushaji zitasaidia kukabiliana na changamoto ya utoshelevu wa walimu kwa ajili ya kufundisha baadhi ya masomo na kuondoa pengo lililopo la kufikisha huduma za kitaaluma kwa wanafunzi.

Upande wake Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Matendo Victor Gideon amesemaa Mradi wa Shule Bora kupitia programu ya Ushirikiano wa Walimu na wazazi shuleni (UWAWA) imeleta mafanikio makubwa ikiwemo kuhamasisha wanafunzi kuhudhuria shule na kuongeza kiwango cha ufaulu kwa shule hiyo.

Amesema kupitia Programu ya Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini(MMEWAKA) pamoja na UWAWA, Shule ya Msingi Kidahwe ilipata jumla ya Shilingi 110,600,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne (4) vya Madarasa na matundu matatu (3) ya vyoo, pamoja na walimu kupatiwa mafunzo kazi ili kuwajengea uwezo

News Bulletin Web: http://www.kigoma.go.tz KIGOMA HABARI ZA MKOA

Toleo Na. 005 Habari za Kila Mwezi 31 Julai 2024

# Tumieni Mabaraza ya Biashara Kupanga Mikakati ya Kibiashara - RC Andengenye

Wafanyabiashara mkoani Kigoma wametakiwa kutumia fursa ya uwepo wa mabaraza ya Biashara kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuibua fursa mpya za kiabiashara badala ya kutumika kwa ajili ya kutatua migogoro ya wafanyabiashara pekee.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Thobias Andengenye alipozungumza wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Biashara Mkoa wa Kigoma uliofanyika katika Hoteli ya Lake Tanganyika iliyopo Manispaa ya Kigoma Ujiji na




*CGF (Mst.) Thobias Andengenye Mkuu wa Mkoa wa Kigoma*

kusisitiza kuwa serikali itaendelea kuimarisha Mazingira ya uwekezaji mkoani Kigoma ili kutimiza dhamira ya Mhe. Rais ya Dkt. Samia Suluhu ya kuufanya mkoa kuwa kitovu cha Biashara kwa ukanda wa Magharibi.

Amesema ili kuleta tija kibiashara mikutano ya mabaraza ya biashara isitumike kutatua changamoto za wafanyabiashara pekee bali iweke mikakati ya pamoja katika kuibua fursa za kibiashara na uwekezaji ili kuinua uchumi wa mkoa na Taifa kwa ujumla.

"Iwapo mikutano hii itafanyika mara kwa mara, itaondoa migogoro isiyo ya lazima na kutuepusha migomo ya wafanyabiashara inayoweza kujitokeza kutokana na changamoto zilizopo kupata utatuzi kwa wakati hii" amesema Andengenye.

Amesema Serikali imeelekeza zaidi ya Shilingi trilioni Nane (8) kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya uchukuzi na usafirishaji mkoani Kigoma sambamba na kufanya ukarabati wa meli za Mt. Sangara, MV Liemba pmaoja na Mwongozo kwa ajili ya kujenga mazingira rafiki kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje ya mkoa wa Kigoma kusafiri wao wenyewe na kusafirisha bidhaa zao.

"Serikali ya awamu ya Sita inaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme wa uhakika wa Gridi ya Taifa , kuboresha uwanja wa ndege pamoja na ujenzi wa barabara zinazouunganisha mkoa na mikoa ya jirani kwa kiwango cha Lami" amesema Mkuu wa Mkoa

Aidha Mwenyekiti wa kikao hicho ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma amesema Serikali itaendelea kupokea na kufanyia kazi maoni ya wafanyabiashara pamoja na kutatua changamoto zao kwa haraka ili kuwawekea mazingira rafiki wafanyabashara na kuwawezesha kufikia malengo waliyojiwekea.



*Wajumbe wa Baraza la Biashara la Mkoa wa Kigoma wakiendelea kujadili hoja mbalimbali*

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 005 Habari za Kila Mwezi 31 Julai 2024

# "Barabara Kasulu-Manyovu ikamilike ifikapo Machi 2025" Dkt. Mpango



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango amemtaka Mkandarasi anayejenga barabara ya Kasulu Manyovu kwa Kiwango cha Lami kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo ifikapo Machi 2025.

Akizungumza na maelfu ya wakazi wa Wilaya ya Buhigwe akiwa katika Siku ya Pili ya ziara yake ya kikazi mkoani Kigoma, Mhe. Dkt. Mpango amesema maendeleo yam Mkoa wa Kigoma yamechelewa kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu bora ya Barabara Maji, Umeme na Huduma nyingine za jamii kwa muda mrefu na kuwataka wananchi kutumia fursa ya kukamilika kwa miundombinu hiyo kujiletea Maendeleo.

Amesema kukamilika kwa barabara hiyo ambayo ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa barabara ya Kabingo-Kasulu hadi Manyovu yenye urefu wa Km 260.6 kutauunganisha mkoa wa Kigoma na Kagera pamoja na nchi jirani ya Burundi na kutoa fursa za kiuchumi kupitia usafirishaji wa bidhaa mbalimbali za kibiashara.

Akizungumza na wakazi wa Wilaya ya Buhigwe kwa nyakati tofauti tofauti, Dkt. Mpango amesema serikali inalenga kuimarisha miundombinu mbalimbali mkoani hapa ili kuufanya mkoa kuwa kitovu cha biashara na uchumi kwa ukanda wa Magharibi

Aidha Makamu wa Rais, amewataka watendaji wa Serikali mkoani hapa kutumia muda mwingi katika kutembelea na kusimamia miradi ya Maendeleo pamoja na kutosita kuchukua hatua dhidi ya watendaji wazembe wanaochelewesha utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

Upande wake Waziri wa Ujenzi Inocent Bashungwa amesema kwa kushirikiana na wasaidizi wake watahakikisha agizo la Makamu wa Rais linatekelezwa kama ilivyopangwa sambamba na miradi mingine ambayo ameelekeza wizara hiyo kufuatilia na kusimamia utekelezaji wake ili iweze kukamilika na kuwaondolea kero wananchi

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 005 Habari za Kila Mwezi 31 Julai 2024

# Makamu wa Rais awaweka Kikaangoni Wenyeviti wa Vijiji Wilayani Uvinza

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango ameuelekeza uongozi wa Serikali mkoani hapa kuwachukulia hatua watumishi watakaobainika kushiriki kuruhusu uingizaji wa mifugo wilayani



Uvinza kinyume cha Sheria na kusababisha ongezeko la migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Dkt. Mpango ametoa kauli hiyo alipozungumza kwa nyakati tofauti na wakazi wa wilaya ya Uvinza akiwa katika ziara yake ya kikazi mkoani hapa ambapo amesema baadhi ya watumishi wa Umma wasio waadilifu wamekuwa wakipokea fedha kinyume na sharia ili kuwaruhusu wafugaji kuingiza mifugo wilayani humo bila kufuata taratibu zilizowekwa na serikali.

"Mamlaka za vijiji zinapaswa kuzingatia Sheria na Kanuni za matumizi bora ya Ardhi pia nakuagiza Mkuu wa Mkoa pamoja na watendaji wako kuchukua hatua dhidi ya wale wote wanaohusika na zoezi hilo bila kuzingatia maelekezo ya serikali kuhusu taratibu za ufugaji kwani nchi haitegemei mifugo pekee" amesema Dkt. Mpango.

Sambamba na hayo kupitia ziara yake makamu wa Rais amekagua ujenzi wa barabara ya Malagarasi, Ilunde hadi Uvinza yenye urefu wa Km. 51.1ambayo ujenzi wake umefikia Asilimia 54 huku ikitarajiwa kukamilika Machi, 2025.

Mara baada ya kukagua mradi huo, Makamu wa Rais amemuelekeza Mkandarasi anayetekeleza mradi huo kuhakikisha anatumia kipindi hiki cha kiangazi kukamilisha maeneo muhimu ya ujenzi wa barabara hiyo bila kuathiri ubora wa kazi.